

Namna ya kutumia chandarua chenye dawa

Chandarua chenye dawa ni njia bora ya kujikinga na ugonjwa wa malaria.

Dawa iliyowekwa kwenye chandarua imethibitishwa kitaalamu kuwa ni salama kwa afya ya watu wote kwenye familia

Kwanini chandarua ni njia bora ya kujikinga na malaria?

- Chandarua chenye dawa kinafukuza na kuuu mbu waenezao ugonjwa wa malaria.
- Chandarua chenye dawa kitakupa usingizi mnono kila siku kwa kuwa hautosumbuliwa na mbu anayeneza ugonjwa wa malaria.

Zingatia: Dawa iliyowekwa kwenye chandarua inauwezo mkubwa wa kufukuza na kuuu mbu anayeneza ugonjwa wa malaria (Anofelesi).

Namna ya kutumia chandarua chenye dawa

Ni muhimu kutumia chandarua chenye dawa kwa usahihi ili kujikinga na mbu waenezao ugonjwa wa malaria. Zingatia yafuatayo unapotumia chandarua chenye dawa:


- Funga chandarua kwenye eneo la juu ya kitanda (kwenye dari au kenchi)
- Unapofunga chandarua hakikisha chandarua kimeshuka chini vya kutosha ili uweze kukichomeka vizuri kwenye godoro/kirago /mkeka.
- Wakati wa kulala chomeka vizuri chandarua chini ya godoro/kirago/mkeka ili mbu waenezao malaria wasipate nafasi ya kupenya ndani ya chandarua
- Hakikisha unalala kwenye chandarua kwa kipindi chote cha mwaka hata kama kuna mbu wachache au kuna joto. Mbu mmoja tu anatosha kukuambukiza malaria
- Kama kuna joto kali, chandarua kitakusaidia sana kwa kua hautohitaji kujifunika shuka itakayokuongezea joto. Hivyobasi chandarua kitakupa usingizi mnono bila usumbufu wowote wa mbu.
- Hakikisha kila mtu kwenye kaya yako analala kwenye chandarua kila siku.

Mambo ya muhimu unayotakiwa kuelimisha jamii kuhusu matumizi sahihi ya vyandarua vyenye dawa

- kila mtu anaweza kujikinga na malaria kwa urahisi kwa kuhakikisha analala kwenye chandarua chenye dawa kila siku
- chandarua ni njia bora ya kujikinga na malaria na kwanini
- dawa iliyowekwa kwenye chandarua ina uwezo mkubwa wa kufukuza na kuuu mbu jike aina ya Anofelesi. Mbu unaowaona ndani au nje ya chandarua chako si mbu wa malaria
- matundu ya chandarua yanaruhusu hewa kupita tu na ni madogo sana kiasi cha kutoweza kupitisha mbu waenezao ugonjwa wa malaria.
- wakati wa joto chandarua kitawasaidia sana kwa kuwa wataweza kulala kwenye chandarua bila kujifunika shuka bila kuwa na usumbufu wowote wa mbu
- Waelekeze namna yakutumia chandarua chenye dawa
- Jadiliana na kuhusu dhana na imani potofu kwa watu wanaodhani vyandarua vyenye dawa ni hatari kwa afya ya binadamu. Waeleze kuwa chandarua chenye dawa kimethibitishwa kitaalam kuwa ni salama kwa afya ya watu wote kwenye familia ikiwemo watoto wachanga.
- Jadiliana nao kuhusu changamoto wanazokutana nazo wanapotumia chandarua

Namna ya kuhakikisha jamii yote inatumia vyandarua vyenye dawa kila siku

- Pita nyumba hadi nyumba ili kuona kama wametundika au hawajatundika vyandarua (Fanya kufanya shughuli hii kwa kusaidiana na wanajamii na viongozi)
- Kama hawajatundika, fahamu kwanini havijatundikwa na wasaidie kutundika vyandarua na waelekeze namna ya kuvitumia.
- Jadiliana nao namna ya kuwasaidia wale wasiokuwa na vyandarua ili nao wapate vyandarua
- Hakikisha wajawazito wote na watoto wachanga wamepata vyandarua vyao kwa kutumia vocha za hati punguzo. Shirikiana na watoa huduma za afya kuwa vocha za hati punguzo na vyandarua vinapatikana kwa urahisi.
- Jadiliana nao kuhusu dhana na imani potofu kwa watu wanaodhani vyandarua vyenye dawa ni hatari kwa afya ya binadamu
- Jadiliana nao kuhusu changamoto wanazokutana nazo wanapotumia vyandarua. Wataje sababu zinazowafanya wasitumie vyandarua, wasaidie kupata ufumbuzi. Kwa mfano, kutojua wapi pakupata chandarua.



Namna ya kutumia chandarua chenye dawa



1. Kama upo tayari kufunga chandarua, hakikisha kipo katikati ya kitanda. Hakikisha umekifunga vizuri. Vyandarua vyote vya duara na pembe nne vimetengenezwa pamoja na kamba kwa ajili ya kufungia.



2. Wakati wa usiku, chomeka chandarua vizuri kwenye godoro au mkeka ili mbu wakose kabisa nafasi ya kupenya.



3. Malaria ni hatari zaidi kwa wajawazito, watoto walio chini ya umri wa miaka 5 na watu wanaoishi na virusi vya UKIMWI. Kila mtu kwenye familia inampasa alale kwenye chandarua chenye dawa kila siku.



4. Unapoamka asubuhi, kunja chandarua vizuri ili kisiharibike.